

Na Fadhili Rashid, Kilosa

Mkuu wa Mkoa Morogoro Steven Kebwe amewapa siku nne wananchi wa kijiji cha Mululu kata ya Kisanga ambao walivamia kwenye maeneo ya Msitu wa hifadhi wa Ukwiva na kufanya makazi pamoja na shughuli zingine za kibinadamu wawe wameondoka na watakaokaidi agizo hilo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Kebwe amewaambia wananchi hao kwenye mkutano wa hadhara kwa kusema kuwa ukweli unauma lakini ndio ukweli wenyewe kuwa baadhi ya wananchi hao waliovamia wanatakiwa kuhama kwenye eneo la hifadhi kabla serikali haijaanza kuchukua sheria kwani eneo hilo lilishapimwa kwa miaka mingi na mipaka yake inatambulika kisheria hivyo serikali itakapotumia gharama kuwaamisha wananchi hao watalazimika kuilipa serikali.

Wakati huo huo Mkuu huyo wa Mkoa ameongeza kusema kuwa mwezi wa sita mwaka huu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa alitoa tangazo la kuwataka wananchi wote wanaoishi na kufanya shughuli zao kwenye maeneo ya hifadhi ya misitu na vyanzo vya maji kuhama mara moja kabla hawajachukuliwa hatua za kisheria hivyo anawashangaa wananchi hao kuendelea kung'ang'ania kwenye hifadhi hiyo.

Aidha Meneja wa Wakala wa Misitu Tanzania {TFS} wilayani kilosa John Olomi alitoa historia fupi ya Hifadhi ya Misitu ya Ukwiva ambapo alisema mnamo mwaka 1954 tangazo la serikali liliutangaza msitu huo unaozungukwa na vijiji 22 kuwa wa hifadhi, na hivi karibuni TFS kushirikiana na maafisa ardhi, maafisa Misitu na viongozi wa vijiji waliufanyia uhakiki msitu huo na kubaini kuwa baadhi ya wananchi wa vijiji wanaishi kwenye eneo la hifadhi na kufanya shughuli zingine hivyo waliwapa tangazo la kuhama kwa kuwapa siku 14, kuanzia tarehe 4 hadi tarehe 18 mwezi wa saba ambapo baadhi yao waliweza kuhama na wengine wamegoma.

Awali baadhi ya wananchi hao walimweleza mkuu wa mkoa huyo kuwa wanaonewa wanapoambiwa wahame kwani wao walianza kuisha miaka mingi iliyopita wakilithi maeneo hayo kutoka kwa wazazi wao.